

AE.596/687/01/74

27 Mei, 2024

Ndugu Wadau,

KUH: RASIMU ZA VIWANGO VYA ZANZIBAR KWA AJILI YA MAONI KWA UMMA

Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) imeandaa rasimu **mbili** za Kamati ya Bidhaa za Nguo na Ngozi, hivyo inaomba maoni kwa umma kabla ya kupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya ZBS na kisha kutangazwa na Gazeti la Serikali.

Viwango hivyo ni: -

- a) **PCD 519-1: 2023 – Textiles — Specification for knitted vests — Part 1: Knitted vests for males**
- b) **PCD 609: 2024 – Textiles — Specification for nylon stretch socks – Knitted sweater - Specification**

Kulingana na taratibu za kuandaa viwango, rasimu za viwango hivyo husambazwa kwa wadau kwa ajili ya kukusanya maoni na mapendekezo. Tunakuomba upitie rasimu za viwango hivyo na kutuma maoni yako ya kiufundi. Mapendekezo ambayo yana marekebisho ya kimaandishi inapaswa kuonyesha mbadala wake kwa kila kifungu husika. Ikiwa utaona inafaa na hakuna maoni, tafadhali tuarifu ipasavyo.

Maoni lazima yajazwe katika fomu iliyo ambatanishwa na kuwasilisha moja kwa moja katika afisi ya ZBS au kwa barua pepe maoni@zbs.go.tz

Tutashukuru kupokea maoni yako kabla ya tarehe **27 Julai, 2024**

Asante.



(Yusuph M. Nassor)
MKURUGENZI MKUU
TAASISI YA VIWANGO
ZANZIBAR.

Mawasiliano yote yafanywe kwa Mkurugenzi Mkuu Taasisi ya Viwango Zanzibar
Barua pepe: info@zbs.go.tz Simu: +255 24 2232225

Zanzibar Bureau of Standards



www.zbs.go.tz



info@zbs.go.tz